Malawi Kuinua Uzalishaji wa Kilimo Kuboresha Lishe

Na Mabvuto Banda

LILONGWE, Malawi, Nov 30 2015 (IPS)- Ikiwa na matatizo ya ukame wa mara kwa mara na mafuriko ambayo yanaathiri kwa kiasi kikubwa uzalishaji wa chakula, Malawi inajikita katika hatua za kuzuia utapiamlo zaidi.

Katika miaka michache iliyopita, Malawi imefanikiwa kupunguza vifo vya watoto wachanga na wa umri wa chini ya miaka mitano. Lakini kupunguza utapiamlo ambao unaathiri wastani wa watoto milioni 1.4, inaendelea kuwa changamoto yenye gharama kubwa nchini humo.

Ripoti ya Serikali ya Malawi, Shirika la Chakula Duniani (WFP) na Mashirika mengine ya Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika ya mwaka, inakadiria kuwa jumla ya gharama ya mwaka mzima inayogharamia utapiamlo kwa watoto ni dola milioni 597 – dalili inayoonyesha kuwa kuna uhaba mkubwa wa chakula na lishe katika mataifa ya kusini mwa Afrika.

Ili kubadili viwango hivyo vya juu vya utapiamlo, Serikali ya Malawi na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) wamekuja na mipango kadhaa yenye lengo la kuongeza uzalishaji wa kikimo ili kuboresha lishe.

Erica Maganga, Katibu Mkuu wa Kilimo, Umwagiliaji na Maendeleo ya Maji, anaiambia IPS kuwa jukumu la kilimo ni kubwa katika kupambana na aina zote za utapiamlo.

“Kuzuia ni bora kuliko kuponya na kilimo kinasaidia kukabiliana na utapiamlo kwa watu wa umri wote na pia kupunguza gharama,” anasema Maganga.

Mwakilishi Mkaazi wa FAO nchini Malawi Florence Rolle anakubaliana na hoja hiyo.

“Sote tunatambua kuwa lishe ni suala kubwa nchini Malawi na kwamba kilimo kina mchango mkubwa wa kuboresha lishe kwa watoto, wanawake na wanaume,â€ Rolle anasema.

“Ni wakati muafaka sasa kubainisha ni programu zipi za kilimo zina uwezekano wa kukabiliana zaidi na utapiamlo,” anaongeza.

Mwaka 2008, FAO na serikali ya Malawi walianza kutekeleza mradi wa Kuboresha Sera za Usalama wa Chakula na Lishe (IFSN). Moja ya maeneo ya mradi huo ilikuwa kuanza kutekeleza mkakati madhubuti wa kutoa elimu ya lishe kwa familia zenye watoto wachanga kati ya miezi 6 hadi 24 ili kuzuia utapiamlo.

Kutokana na msaada kutoka Shirika la “Flanders International Cooperation Agency (FICA)”, mpango huo ulilenga wilaya mbili — Kasungu, kilomita 100 tu kutoka mji mkuu wa Malawi wa Lilongwe na Mzimba kaskazini mwa Malawi.

Kwa mujibu wa Soka Chitaya, Meneja Miradi wa Wilaya ya Kasungu, mpango huo umekuwa na mafanikio makubwa katika kuboresha afya ya watoto wengi katika wilaya.

“Kabla mradi haujaanza, watoto wengi wachanga walikuwa wakipata maradhi. Mama ambao wengi wao ni wakulima, walikuwa na changamoto ambayo iliathiri shughuli zao za shambani kutokana na kuwa walitumia muda mwingi zaidi kulea watoto wao waliokuwa wagonjwa kuliko kushughulikia bustani zao,” Chitaya anasema.

Lakini anasema kwa sasa habari ni tofauti.

Kondwani Phiri, 32, kutoka Kijiji cha Yosefe, mama wa watoto wanne hana cha kusema zaidi ya kuupongeza mradi.

“Mradi huu ulibadili maisha yangu. Watoto wangu wana afya na furaha kutokana na kuwa sasa nataka kupanda bustani yangu ili kuwa na chakula chenye lishe bora kwa familia,” Phiri aliiambia IPS wakati alipokuwa akiandaa chakula kwa ajili ya mtoto wake katika jua kali la mwezi Novemba.

Lakini ana mashaka kuwa kama mvua zitachelewa mwaka huu, anaweza kupoteza mafanikio yote aliyopata katika miaka michache iliyopita.

Malawi ni miongoni mwa mataifa ya Afrika ambayo yametabiriwa kuja kukabiliwa na ukame katika mikoa ya kati na mafuriko katika mikoa ya kusini kutokana na hali ya hewa ya El Nino.

Loveness Matola, mama mwingine mwenye furaha anatarajia kuwa na mwaka mgumu kutokana na mvua kuwa zimeshachelewa, lakini ana matumaini ataweza kulima na kuwa na chakula cha kutosha kwa ajili ya familia. “Mpango huu umesaidia kuingiza watoto wangu wachanga katika Mpango Lishe wa Watoto Wadogo. Sina wasiwasi tena wa jinsi ya kulima chakula chenye lishe katika bustani yangu,” alisema.

Kutokana na kupata msaada kutoka kwa Maafisa Ugani, Wafanyakazi wa Afya na Wawezeshaji katika Jamii, Phiri na Matola, pamoja na mama wengine, wamejifunza jinsi ya kutengeneza uji wa lishe unaotokana na mazao aina tatu kutoka shambani.

Uji huo una wanga kama vile viazi mviringo, mihogo au mahindi, protini ya hali inayotokana maharage, karanga, samaki au nyama au maziwa ya mbuzi pamoja na mbogamboga kama vile maboga au mboga za majani na mafuta kama vile mafuta ya parachichi. Maembe au tunda jingine lolote lile linatumika kukamilisha mlo wa siku wa mtoto mchanga.

Miongoni mwa maeneo mengine yanayolengwa, mradi unakuza uzalishaji wa mifugo; mabadiliko ya tabia nchi, elimu ya rasilimali na mazingira; kujenga uwezo wa kitaasisi; kuongeza uzalishaji wa mazao na kupanda mazao mseto; kukuza kilimo cha matunda; hifadhi ya udongo na maji; maji ya bomba na uboreshaji wa huduma za vyoo na maliwato, na masuala mengine mtambuka kama vile jinsia, Malaria na VVU.

Huu siyo mradi pekee ambao FAO na serikali ya Malawi wanafanya katika kuboresha lishe nchini.

“Mradi wa Kuboresha Elimu ya Lishe na Bustani Mashuleni” pia unatekelezwa.

Serikali ya Malawi, FAO na serikali ya Brazili walisaini mkataba wenye maeneo makuu yafuatayo: kuboresha Mkakati wa Afya na Lishe Mashuleni, Elimu ya Lishe na Kuunganisha Elimu ya Lishe na ile ya Bustani.

Mtaalam wa FAO wa masuala ya Chakula na Lishe Mashuleni, Dk Andrea Polo Galante alielezea mpango huo kuwa una lengo la kuboresha elimu ya lishe, ambayo inalenga katika kuzalisha chakula zaidi na kula vizuri.

Kwa mujibu wa Thoko Banda, Mkurugenzi Mkuu wa Wizara ya Elimu, tathmini hiyo inafanyika kutoa mapendekezo ya kuingiza suala hilo katika Mafunzo ya Vyuo vya Ualimu.

(End)